قَالَ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ:

# "إِنَّهُ مَنْ لَمْ يَسْأَلِ اللَّهَ يَغْضَبْ عَلَيْهِ"

## "HAKIKA YULE ATAKAYEACHA KUMUOMBA ALLAAH, (ALLAAH) ATAMGHADHIBIKIA". (Tirmidh: 3373).

NA MSHAIRI ANASEMA:

اللهُ يَغْضَبُ إِنْ تَرَكْتَ سُؤَالَهُ ** وَبُنَيُّ آدَمَ حِينَ يُسْأَلُ يَغْضَبُ

ALLAAH ANACHUKIA UKIACHA KUMUOMBA ** LAKINI BINADAMU UKIMUOMBA ANACHUKIA

Mwandishi:

Abu Halima Arafat Bin Mahmoud

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kila sifa njema anastahiki Allaah Ta'alaa, na-Swala na Salamu zimshukie-Mtume wetu Muhammad, Jamaa zake na Maswahaba wake wote.

Baada ya hayo: Hakika Allaah Subhaanah katika Aya nyingi ndani ya Qur'an amewaamrisha waja wake kumuomba Yeye na akawaahidi kuwaitikia[1]:

﴿وَقَالَ رَبُّكُمُ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ ۚ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ﴾

**"Na Mola wenu Mlezi amesema: Niombeni nitakuitikieni. Hakika wale ambao wanafanya kibri kuacha kuniomba mimi wataingia Jahannam hali ya kuwa madhalili"[2].**

Na amtume-Swala na Salamu zimshukie-:

"لَيْسَ شَيْءٌ أَكْرَمَ عَلَى اللهِ تَعَالَى مِنَ الدُّعَاءِ"

**"Hakuna ibada iliyo bora zaidi mbele za Allaah kuliko Dua"[3].**

Na amesema tena:

"إِنَّهُ مَنْ لَمْ يَسْأَلِ اللَّهَ يَغْضَبْ عَلَيْهِ"

**"Hakika yule atakayeacha kumuomba Allaah, (Allaah) atamghadhibikia"[4].**

Na Imam Ibnul Qayyim-Allaah amrehemu- amekusanya ufupisho mzuri, na amebainisha ndani yake mambo ya msingi ambayo inampasa mwenye kuomba Dua kuyazingatia, kisha baada ya kutaja masharti hayo akasema:

"فَإِنَّ هَذَا الدُّعَاءَ لَا يَكَادُ يُرَدُّ أَبَدًا"

**"Hakika Dua hii ni mara nyingi kukubaliwa"[5].**

**Wallaahu A'lam.**

---

1- Makala ni sehemu ya Risala yetu inayoitwa DUA ISIYOKATALIWA ambayo tumeifanyi tarjama mwaka 1442h – 2021m..
2- Surat Ghafir/60.
3- Sunan Tirmidh (3370).
4- Sunana Tirmidh (3373).
5- Kitabu: [Al Jawaabul Kaafi] (Uk. 9).

## JAMBO LA KWANZA

## KUHUDHURIA KWA MOYO NA KUKUSANYIKA KWENYE LILE UNALOLIOMBA

Amesema Mtume-Swala na Salamu zimshukie-:

" وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ لاَ يَسْتَجِيبُ دُعَاءً مِنْ قَلْبٍ غَافِلٍ لاَهٍ "

**"Na tambueni kwamba Allaah hajibu dua yoyote kutoka kwenye moyo wenye kughafilika (moyo) wenye pumbao"[6].**

Kadhalika Umar Bin Abdil Azizi-Allaah amrehemu- alimuona mtu mmoja anaomba dua, hali ya kuwa mkononi mwake ameshika mawe (changarawe) anachezea, akamwambia:

" أَلَا أَلْقَيْتَ الْحَصَاةَ، وَأَخْلَصْتَ إِلَى اللهِ الدُّعَاءَ؟ "

**"Kwanini usitupe hayo mawe, na ukamuelekea Allaah kwa kumuomba Dua?"[7].**

## JAMBO LA PILI

## KUWA TWAHARA WAKATI WA KUOMBA DUA

Hii ni miongoni mwa adabu za kuomba Dua, kwani inapendeza muombaji wakati wa kumuomba Allaah awe twahara na udhu ulio kamili.

Imepolewa kutoka kwa swahaba Muhajir Bin Qunfudh-Allaah amridhie-kwamba yeye alimuona Mtume-Swala na Salamu zimshukie- anatawadha, alipomsalimia Mtume hamuitikia, alipomaliza kutawadha alimwambia:

" إِنَّهُ لَمْ يَمْنَعْنِي أَنْ أَرُدَّ عَلَيْكَ إِلَّا أَنِّي كَرِهْتُ أَنْ أَذْكُرَ اللهَ إِلَّا عَلَى طَهَارَةٍ "

**"Hakuna kilichonizuia mimi kuitikia (salamu yako) isipokuwa nimeona karaha kumdhukuru Allaah isipokuwa niwe katika twahara"[8].**

---

6- Sunan Tirmidh (3479).
7- Kitabu: [Hilyatul Auliyaa] (Jz. 5, Uk. 287).
8- Kitabu: [Musnad Ahmad] (19034).

## JAMBO LA TATU

## UNYENYEKEVU WA MOYO NA KUDHALILIKA KWAKE MBELE YA ALLAAH

Allaah anasema:

﴿ ٱدۡعُواْ رَبَّكُمۡ تَضَرُّعٗا وَخُفۡيَةًۚ إِنَّهُۥ لَا يُحِبُّ ٱلۡمُعۡتَدِينَ ﴾

**"Mwombeni Mola Mlezi kwa unyenyekevu na kwa siri. Hakika yeye hawapendi wenye kuvuka mipaka"(9).**

Amesema Imamu Twabari-Allaah amrehemu- wakati akifafanua Aya hii:

" تَذَلُّلًا وَاسْتِكَانَةً لِطَاعَتِهِ، بِخُشُوْعِ قُلُوْبِكُمْ، لَا جِهَارًا وَمُرَاءَاةً "

**"Kwa udhalili na unyenyekevu wa mioyo yenu kwa ajili ya kumtii yeye, si kwa kudhihirisha sauti"(10).**

Mtume -Swala na Salamu zimshukie- aliwaona baadhi ya Maswahaba Allaah awaridhie wakinyanyua sauti zao wakisoma dhikri na dua, akasema:

«أَيُّهَا النَّاسُ ارْبَعُوا عَلَى أَنْفُسِكُمْ، إِنَّكُمْ لَيْسَ تَدْعُونَ أَصَمَّ وَلَا غَائِبًا، إِنَّكُمْ تَدْعُونَ سَمِيعًا قَرِيبًا»

**"Enyi watu, jihurumieni nafsi zenu, hakika hamkuwa nyinyi mnamuomba kiziwi wala aliye mbali, hakika mnamuomba Mwenye kusikia Aliye karibu…"(11).**

Amesema Ibn Hajar-Allaah amrehemu-: **"Amesema At Twabary:**

" فِيهِ كَرَاهِيَةُ رَفْعِ الصَّوْتِ بِالدُّعَاءِ وَالذِّكْرِوَبِهِ قَالَ عَامَّةُ السَّلَفِ مِنَ الصَّحَابَةِ وَالتَّابِعِينَ "

**"Kuna katika hadithi hii karaha ya kunyanyua sauti wakati wa kuomba Dua, na hivyo ndivyo walivyosema (Maulamaa) wote wa Salaf katika Maswahaba na Taabiin"(12).**

Imam An Nawawi-Allaah amrehemu- ameiwekea hadithi hii mlango:

" بَاب اسْتِحْبَابِ خَفْضِ الصَّوْتِ بِالذِّكْرِإِلَّافِي الْمَوَاضِعِ الَّتِيْ وَرَدَ الشَّرْعُ بِرَفْعِهِ فِيْهَا "

**"Huu ni mlango wa kupendekezwa kuteremsha sauti kwa ajili kusoma Adhkaar, isipokuwa sehemu ambazo sheria imeidhinisha kunyanyua sauti katika sehemu hizo"(13).**

---

9- Surat Al A'raaf/55.
10- Kitabu: [Jaamiu al bayaan fiy Tafsiir al Qur'an] (Jz. 12, Uk. 485).
11- Bukhari (2992) na Muslim (2704), na hili ni tamko la Imam Muslim.
12- Kitabu: [Fat-hu al Baari] (Jz. 6, Uk. 135).
13- Kitabu: [Sharhu Muslim] (Jz. 17, Uk. 25).

## JAMBO LA NNE

## KUPATILIZA NYAKATI AMBAZO DUA HUJIBIWA KWA HARAKA

Nyakati hizo ni kama alivyosema Imam Ibnul Qayyim-Allaah amrehemu-:

### 1. Thuluthi ya mwisho ya usiku:

**" يَنْزِلُ رَبُّنَا تَبَارَكَ وَتَعَالَى كُلَّ لَيْلَةٍ إِلَى السَّمَاءِ الدُّنْيَا حِينَ يَبْقَى ثُلُثُ اللَّيْلِ الآخِرُ يَقُولُ: مَنْ يَدْعُونِي، فَأَسْتَجِيبَ لَهُ مَنْ يَسْأَلُنِي فَأُعْطِيَهُ، مَنْ يَسْتَغْفِرُنِي فَأَغْفِرَ لَهُ "**

**"Mola wetu aliyetukuka anateremka kila usiku mpaka kwenye mbingu (iliyo karibu na) dunia, wakati inapobaki thuluthi ya mwisho ya usiku, anasema: Nani anayeniomba ili nimjibu?, Nani anayeniomba mimi kitu ili nimpatie?, Nani anayeniomba msamaha ili nimsamehe?".** [Bukhari (1145) na Muslim (758)].

### 2. Baada tu ya kumalizika Adhana:

Mtume-Swala na Salamu zimshukie- alimwambia swahaba mmoja:

**«قُلْ كَمَا يَقُولُونَ فَإِذَا انْتَهَيْتَ فَسَلْ تُعْطَهْ»**

**"Itikia kama wanavyosema (waadhini), na utakapomaliza Omba utapewa"[14].[15]**

### 3. Wakati wa baina ya Adhana na Iqama:

Amesema Mtume-Swala na Salamu zimshukie-:

**«لَا يُرَدُّ الدُّعَاءُ بَيْنَ الْأَذَانِ وَالْإِقَامَةِ»**

**"Dua baina ya Adhana na Iqama hairudishwi".** [Sunan Abi Daud (4913)].

Na anasema:

**«إِذَا نُودِيَ بِالصَّلَاةَ، فُتِحَتْ أَبْوَابُ السَّمَاءِ، وَاسْتُجِيبَ الدُّعَاءُ»**

**"Inapoadhiniwa adhana kwa ajili ya swala, milango ya mbingu hufunguliwa na Dua hujibiwa"[16].**

---

[14]- Sunan Abi Daud (524) Daraja lake ni Hasan.

[15]- Kuna sunna tano kwa mtu mwenye kusikia Adhana:

I. kumuitikia muadhini kama anavyosema isipokuwa katika حَيَّ الصَّلَاةِ na حَيَّ عَلَى الفَلَاحِ utasema: لَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ

II. Baada ya Adhana kumalizika utamswalia Mtume: اللهم صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ محمد كما صَلَّيْتَ على إبراهيمَ وعلى آل إبراهيم...

III. Kisha utaomba Dua: اللهُمَّ رَبَّ هَذِهِ الدَّعْوَةِ التَّامَّةِ، والصَّلَاةِ الْقَائِمَةِ، آتِ مُحَمَّدًا الوَسِيْلَةَ وَالْفَضِيْلَةَ، وَ ابْعَثْهُ مَقَامًا مَحْمُوْدًا الَّذِيْ وَعَدتَّهُ

IV. Kisha utasoma: أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وحده لا شريك له، وأن محمدا عَبْدُهُ ورَسُولُهُ، رَضِيْتُ بِاللهِ رَبًّا، وَبِمُحَمَّدٍ رسُوْلًا، وَبِالْإِسْلَام دِيْنًا

V. Kisha utaomba Dua utakayo.

[16]- Kitabu: [Musnad Twayaalis] (524), pia tazama kitabu: [As Sahiha] (1413).

### 4. Mwishoni mwa swala ya faradhi:

Mtume-Swala na Salamu zimshukie- alimfundisha swahaba Abdullah Ibn Masoud-Allaah amridhie- Tashahhud/At Tahiyyaat, kisha akamwambia:

" ثُمَّ يَتَخَيَّرُ مِنَ الدُّعَاءِ أَعْجَبَهُ إِلَيْهِ، فَيَدْعُو "

**"Kisha achague katika Dua ile inayopendeza zaidi kwake aombe"(17).**

### 5. Imam akiwa juu ya mimbari siku ya Ijumaa, mpaka kumalizika swala:

Ushahidi ni hadithi inayosema:

«إِنَّ فِي الْجُمُعَةِ لَسَاعَةً، لَا يُوَافِقُهَا مُسْلِمٌ، قَائِمٌ يُصَلِّي، يَسْأَلُ اللهَ خَيْرًا، إِلَّا أَعْطَاهُ إِيَّاهُ»

**"Hakika siku ya Ijumaa kuna muda (mdogo) ambao haudiriki muislamu yeyote, hali ya kuwa ni mwenye kulazimiana na kuomba Dua, na kumuomba Allaah kheri, isipokuwa Allaah atampa hilo (analoomba)"(18).**

Baadhi ya Maulamaa wanasema wakati huo ni baada ya Imam kupanda juu ya mimbari mpaka kukamilika kwa swala ya Ijumaa, kwa hadithi ya Abu Musa-Allaah amridhie-:

«هِيَ مَا بَيْنَ أَنْ يَجْلِسَ الْإِمَامُ إِلَى أَنْ تُقْضَى الصَّلَاةُ»

**"(Wakati huo) ni baina ya kukaa Imam juu ya mimbari mpaka kuswaliwa Ijumaa"(19).**

### 6. Baada ya swala ya alasiri mpaka kuzama kwa jua siku Ijumaa:

Imekuja katika hadithi kwamba siku ya Ijumaa kuna wakati ambao muislamu akimuomba Allaah kitu chochote atampatia, Mtume-Swala na Salamu zimshukie- akasema:

« فَالْتَمِسُوهَا آخِرَ سَاعَةٍ بَعْدَ الْعَصْرِ»

**"Utafuteni muda huo wakati wa mwisho baada ya swala ya alasiri"(20).**

---

17- Bukhari (835) na Muslim (402) na tamko hili ni la Imam Muslim.
18- Bukhari (6400) na Muslim (852), na tamko hili ni la Muslim.
19- Muslim (482).
20- Sunan Abi Daud (1048).

## JAMBO LA TANO

## KUELEKEA UPANDE WA KIBLA WAKATI WA KUOMBA DUA

Kuelekea upande wa kibla wakati wa kuomba Dua huzingatiwa ni miongoni mwa adabu za Dua, na inafahamisha namna gani mwombaji anamuadhimisha Mola wake, kama ilivyothibiti kwamba Mtume-Swala na Salamu zimshukie- siku ya vita vya Badr, wakati alipoona idadi kubwa ya jeshi la washirikina…

" فَاسْتَقْبَلَ نَبِيُّ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ الْقِبْلَةَ، ثُمَّ مَدَّ يَدَيْهِ "

**"Mtume wa Allaah -Swala na Salamu zimshukie- akaelekea kibla, kisha akainua mikono yake"(21).**

## JAMBO LA SITA

## KUNYANYUA MIKONO WAKATI WA KUOMBA DUA

Imepokewa kutoka kwa Salmaan Al Faarisy -Allaah amridhie-, kwamba Mtume-Swala na Salamu zimshukie- amesema:

«إِنَّ رَبَّكُمْ تَبَارَكَ وَتَعَالَى حَيِيٌّ كَرِيمٌ، يَسْتَحْيِي مِنْ عَبْدِهِ إِذَا رَفَعَ يَدَيْهِ إِلَيْهِ، أَنْ يَرُدَّهُمَا صِفْرًا»

**"Hakika Mola wenu Mlezi ni Mwenye kuona haya na Mkarinu, anamuonea haya mja wake pindi akinyanyua(22) mikono kuielekeza kwake kuirudisha sifuri (patupu)"(23).**

Na siku moja akiwa juu ya mimbari alipoomba Dua ya kunyeshelezwa mvua, anasimulia Anas Ibn Malik-Allaah amridhie-:

«رَأَيْتُ رَسُولَ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَرْفَعُ يَدَيْهِ فِي الدُّعَاءِ، حَتَّى يُرَى بَيَاضُ إِبْطَيْهِ»

**"Nilimuona Mtume -Swala na Salamu zimshukie- ananyanyua mikono yake katika kuomba Dua, mpaka unaonekana weupe wa kwapa zake"(24).**

Ikiwa ni Dua ya kawaida utanyanyua mikono yako mpaka usawa wa mabega yako, na kama ni Dua ya majanga utanyanyua mikono juu zaidi.

---

21- Muslim (1763).

22- Hii ni miongoni mwa dalili kwamba yuko juu, kwa sababu mwenye kuomba Dua ananyanyua mikoni yake kuelekeza mbinguni.

23- Sunan Abi Daud (1488).

24- Bukhari (1030) na Muslim (895), na tamko hili ni la Imam Muslim.

## JAMBO LA SABA

### KUANZA KWA KUMSIFU ALLAAH NA KUMTUKUZA, KISHA KUMSWALIA MTUME صلى الله عليه وسلم

Mtume-Swala na Salamu zimshukie- amesema:

**«إِذَا صَلَّى أَحَدُكُمْ، فَلْيَبْدَأْ بِتَمْجِيدِ رَبِّهِ جَلَّ وَعَزَّ، وَالثَّنَاءِ عَلَيْهِ، ثُمَّ يُصَلِّي عَلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، ثُمَّ يَدْعُو بَعْدُ بِمَا شَاءَ»**

**"Ataposwali mmoja wenu, aanze kumtukuza Mola wake 'Azza Wajalla na kumsifu, kisha amswalie Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, baada ya hapo aombe anachotaka"[25].**

## JAMBO LA NANE

### KUTANGULIZA TOBA NA ISTIGHFAAR KABLA YA KUOMBA DUA

Madhambi ni moja ya kizuizi cha kutojibiwa, kama ilivyokuja katika hadithi ambayo Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alimtaja mtu mmoja akasema:

**" يُطِيلُ السَّفَرَ أَشْعَثَ أَغْبَرَ، يَمُدُّ يَدَيْهِ إِلَى السَّمَاءِ، يَا رَبِّ، يَا رَبِّ، وَمَطْعَمُهُ حَرَامٌ، وَمَشْرَبُهُ حَرَامٌ، وَمَلْبَسُهُ حَرَامٌ، وَغُذِيَ بِالْحَرَامِ، فَأَنَّى يُسْتَجَابُ لِذَلِكَ؟ "**

**"Amesafiri safari ndefu, hali kuwa ametimka nywele zake, amejaa vumbi, hali ya kuwa amenyanyua mikono yake kuelekeza mbinguni, (anamuomba Mola wake akisema): Yaa Rabbi Yaa Rabbi (Ewe Mola wamu Mlezi), hali ya kuwa chakula chake ni haramu, kinywaji chake ni haramu, nguo zake ni za haramu, na amekulia kwa haramu, basi kutokea wapi atajibiwa mtu huyo! "[26].**

Amesema Yahya Bin Muadh Ar Raazi-Allaah amrehemu-:

**" لَا تَسْتَبْطِئَنَّ الْإِجَابَةَ إِذَا دَعَوْتَ وَقَدْ سَدَدْتَ طُرُقَهَا بِالذُّنُوبِ "**

**"Usione kuchelewa kujibiwa pindi ukiomba, hali ya kuwa umeziba njia zake kwa sababu ya madhambi"[27].**

---

25- Sunan Abi Daud (1481) na Tirmidh (3477).
26- Muslim (1015).
27- Kitabu: [Shu'abu al Imaan] (1154).

## JAMBO LA TISA

### KUBEMBELEZA NA KUTOKATA TAMAA WALA KUHARAKISHA KUJIBIWA

Imepokewa kutoka kwa Abu Huraira-Allaah amridhie-, kwamba Mtume-Swala na Salamu zimshukie- amesema:

" يُسْتَجَابُ لِأَحَدِكُمْ مَا لَمْ يَعْجَلْ، فَيَقُولُ: قَدْ دَعَوْتُ رَبِّي فَلَمْ يَسْتَجِبْ لِي "

**“Hujibiwa mmoja wenu muda wa kuwa hajakata tamaa, (mpaka) akawa anasema: Nimemuomba Mola wangu wala hajanijibu”(28).**

Amesema Ibnul Qayyim-Allaah amrehemu-:

" وَمِنَ الْآفَاتِ الَّتِي تَمْنَعُ تَرَتُّبَ أَثَرِ الدُّعَاءِ عَلَيْهِ: أَنْ يَسْتَعْجِلَ الْعَبْدُ، وَيَسْتَبْطِئَ الْإِجَابَةَ، فَيَسْتَحْسِرُ وَيَدَعُ الدُّعَاءَ"

**“Miongoni mwa vizuizi ambavyo vinazuia kupatikana athari ya Dua yake ni: mtu kuharakisha, na kuona anachelewa kujibiwa, matokeo yake anakata tamaa na kuacha kuomba Dua”(29).**

## JAMBO LA KUMI

### KUTANGULIZA KUTOA SADAKA KABLA KUOMBA DUA

Sadaka ina athari kubwa kwenye kukubaliwa Dua ya mwombaji.

Mtume-Swala na Salamu zimshukie- amesema:

«وَصَدَقَةُ السِّرِّ تُطْفِئُ غَضَبَ الرَّبِّ»

**“Na sadaka anayoitoa mtu kwa siri inazima hasira za Mola Mlezi”(30).**

Na kutoa sadaka ni miongoni mwa amali njema ambazo inajuzu kwa muislamu kutawasali kwazo wakati akiomba Dua, mfano akasema: **Ewe Mola wangu, ikiwa mimi nilitoa sadaka fulani (ataitaja) kwa ajili yako, naomba nipatie kitu fulani au niondelee kitu fulani (atakitaja)** n.k.

---

28- Bukhari (6340) na Muslim (2735).
29- Kitabu: [Al Jawaabu al Kaafi] (Uk. 15).
30- Kitabu: [Al Mu'jamu al Kabir] (8014).

## JAMBO LA KUMI NA MOJA
## AKUSANYE KATIKA DUA YAKE BAINA YA MATUMAINI NA KHOFU

Allaah alipotaja visa vya Mitume katika surat Al Anbiyaa, na namna alivyowaokoa na vitimbi na kuwanusuru na mitihani mbalimbali akasema:

﴿وَٱلَّذِينَ يُؤۡتُونَ مَآ ءَاتَواْ وَّقُلُوبُهُمۡ وَجِلَةٌ أَنَّهُمۡ إِلَىٰ رَبِّهِمۡ رَٰجِعُونَ﴾

**"Na wale ambao wanatoa walichopewa na hali ya kuwa nyoyo zao zinaogopa kwa kuwa watarejea kwa Mola wao Mlezi"(31).**

Wanajitahidi katika kufanya amali njema wakiwa na matumaini ya kupata ujira mbele ya Allaah, pamoja na hayo mioyo yao ina khofu zisije kukataliwa amali zao.

Na mfano wake ni pale Nabii Ibrahim -Alayhis-Swalaatu was-Salaam-, pamoja na utukufu na cheo chake mbele ya Allaah, tena anaijenga (Al ka'ba), lakini alipomaliza alisema:

﴿رَبَّنَا تَقَبَّلۡ مِنَّآۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلسَّمِيعُ ٱلۡعَلِيمُ﴾

**"Ewe Mola wangu Mlezi, Tutakabalie. Hakika wewe ni Msikivu Mjuzi"(32).**

Ndio maana Wuhaib Bin Wardi-Allaah amrehemu- alipoisoma aya hii alilia, kisha akasema:

" يَا خَلِيلَ الرَّحْمَنِ، تَرْفَعُ قَوَائِمَ بَيْتِ الرَّحْمَنِ وَ أَنْتَ مُشْفِقٌ أَنْ لَا يَتَقَبَّلَ مِنْكَ "

**"Ewe kipenzi cha Allaah Mwingi wa Rehma, unajenga msingi wa nyumba ya Allaah Mwingi wa rehma, na hali ya kuwa unachelea huenda hatoitakabali (amali yako)"(33).**

---

31- Surat Al Mu'minin/60.
32- Surat Al Baqara/127.
33- Kitabu: [Tafsi Ibn Kathir] (Jz. 1, Uk. 247).

## JAMBO LA KUMI NA MBILI
## KUJIKURUBISHA KWA ALLAAH KWA MAJINA NA SIFA ZAKE TUKUFU

Allaah anasema:

﴿وَلِلَّهِ ٱلْأَسْمَآءُ ٱلْحُسْنَىٰ فَٱدْعُوهُ بِهَا﴾

**"Na ana Allaah majina mazuri. Basi mwombeni kwayo"(34).**

Kwa sababu zimekuja Dua mbalimbali kutoka Mtume na Manabii waliopita kabla yake-Alaihimus Swalaatu was Salaam-, wakijikurubisha kwa Allaah kwa kutaja majina au sifa zake . Imekuja kwenye Dua ya Nabii Shuaib-:

﴿رَبَّنَا ٱفْتَحْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ قَوْمِنَا بِٱلْحَقِّ وَأَنتَ خَيْرُ ٱلْفَٰتِحِينَ﴾

**"Ewe Mola wetu Mlezi, tuhukumie baina yetu na jamaa zetu kwa haki, nawe ndiye mbora wa wenye kuhukumu"(35).**

Kadhaalika Nabii Issa-Alaihis Swaatu was Salaamu-:

﴿وَٱرْزُقْنَا وَأَنتَ خَيْرُ ٱلرَّٰزِقِينَ﴾

**"Basi turuzuku, nawe ndiye mbora wa wanaoruzuku"(36).**

Mtume-Swala na Salamu zimshukie- alimsikia mtu mmoja anomba Dua akisema:

**اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ أَنِّي أَشْهَدُ أَنَّكَ أَنْتَ اللَّهُ، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، الْأَحَدُ الصَّمَدُ الَّذِي لَمْ يَلِدْ، وَلَمْ يُولَدْ، وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ. فقال: «لَقَدْ سَأَلْتَ اللَّهَ بِالِاسْمِ الَّذِي إِذَا سُئِلَ بِهِ أَعْطَى، وَإِذَا دُعِيَ بِهِ أَجَابَ».**

**[Ewe Allaah, hakika mimi nakuomba wewe (kwa kutawasali kwako), kwa sababu ninashuhudia kwamba wewe ndiye Allaah Muabudiwa, Hapana Muabudiwa wa haki isipokuwa wewe. Uliye mmoja Mwenye kukusudiwa (na waja) katika haja zote, ambaye hakuzaa wa hakuzaliwa, na wala hakuna kitu chochote ni mfano kwake yeye]. "Akasema: "Hakika umemuomba Allaah kwa jina ambalo akiombwa Dua kwa jina hilo anajibu na akiombwa kitu anatoa"(37).**

---

34- Surat Al A'raaf/180.
35- Surat Al A'raaf/89.
36- Surat Al Maida/114.
37- Sunan Abi Daud (1493).

## JAMBO LA KUMI NA TATU

## KUOMBA DUA ZAKO UKICHANGANYA PAMOJA NA DUA ZAKO HUJIBIWA KWA HARAKA

Mfano Dua ya Nabii Yunus -Alaihis Swalaatu was Salaamu- aliyoiomba akiwa tumboni mwa Chewa, akasema:

﴿لَّآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنتَ سُبۡحَٰنَكَ إِنِّي كُنتُ مِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ﴾

**"Hapana Muabudiwa wa haki isipokuwa wewe, kutakasika na makosa ni kwako. Hakika nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu"[38].**

Amesema Mtume-Swala na Salamu zimshukie-:

**"دَعْوَةُ ذِي النُّونِ إِذْ دَعَا وَهُوَ فِي بَطْنِ الحُوت.. فَإِنَّهُ لَمْ يَدْعُ بِهَا رَجُلٌ مُسْلِمٌ فِي شَيْءٍ قَطُّ إِلاَّ اسْتَجَابَ اللَّهُ لَهُ"**

**"Dua ya Dhin Nun (Nabii Yunus) wakati alipoomba hali ya kuwa yumo tumboni mwa Chewa……., hakika hatoomba kwa Dua hiyo muislamu yeyote kwenye dhiki yoyote, isipokuwa Allaah atamuitikia"[39].**

Mtume-Swala na Salamu zimshukie- alimsikia mtu mmoja akisoma Dua:

**" اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِأَنَّ لَكَ الْحَمْدُ، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ الْمَنَّانُ، بَدِيعُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ، يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ، يَا حَيُّ يَا قَيُّومُ "**

**"Ewe Allaah, hakika mimi nakuomba wewe (kheri kwa kutawasali na kukusifu wewe), kwa sababu ni zako wewe tu sifa njema zote. Hapana Muabudiwa wa haki ila wewe, Mwenye kipawa (kutoa), Muumba wa mbingu na ardhi, Ewe Mwenye utukufu na ukarimu, Ewe uliye hai mwenye kusimamia kila kitu".**

Akasema Mtume-Swala na Salamu zimshukie-

**«لَقَدْ دَعَا اللَّهَ بِاسْمِهِ الْعَظِيمِ، الَّذِي إِذَا دُعِيَ بِهِ أَجَابَ، وَإِذَا سُئِلَ بِهِ أَعْطَى»**

**"Hakika amemuomba Allaah kwa jina tukufu, ambalo akiombwa kwa jina hilo anajibu, na akiombwa kitu kwa jina hilo anatoa"[40].**

**Wabillaah Ttaufiq.**

**18/Ramadhani/1445H – 28/3/2024M.**
**Pongwe Tanga.**

---

38- Surat Al Anbiyaa/87.
39- Sunan Tirmidh (3505) na Ahmad (1462).
40- Sunan Abi Daud (1495). Mtu huyo anaitwa Abu Ayyash Zaid Bin Swamit Az Zuraqi -Allaah amridhie-.